



**AZIMIO NA. 3/2014**

**AZIMIO LA KURIDHIA ITIFAKI YA KUANZISHA UMOJA WA FEDHA  
WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (PROTOCOL ON THE  
ESTABLISHMENT OF THE EAST AFRICAN COMMUNITY MONETARY  
UNION)**

**KWA KUWA** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (East African Community) kwa mujibu wa Mkataba ulioanzisha Jumuiya hii ambao ulisainiwa na Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki tarehe 30 Novemba, 1999;

**NA KWA KUWA** Mkataba huu unazitaka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kushirikiana katika nyanja mbalimbali ili kuleta maendeleo kwa misingi ya haki, usawa na faida kwa wote;

**NA KWA KUWA** Mkataba unaelekeza kwamba kila Itifaki itakayoandaliwa itaidhinishwa na mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na itapaswa kusainiwa na kuridhiwa na Nchi Wanachama;

**NA KWA KUWA** Itifaki ya kuanzisha Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (Protocol on the Establishment of the East African Community Monetary Union) ilitiwa saini na Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya tarehe 30 Novemba, 2013 mjini Kampala, Uganda;

**NA KWA KUWA** Tanzania ni mojawapo ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilizotia saini Itifaki hii, ambapo kwa mujibu wa Ibara ya 30 ya Itifaki ya kuanzisha Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, inawajibika kuridhia Itifaki hii ili kuruhusu utekelezaji wake;

**NA KWA KUWA** kwa kujiunga na Itifaki hii, Tanzania itafaidika kutokana na kupungua kwa gharama ya kufanya biashara katika Nchi Wanachama na hivyo kuhamasisha ukuaji wa biashara baina ya Tanzania na Nchi Wanachama, kuwezesha Tanzania kuwa na kiwango kidogo na tulivu cha mfumuko wa bei na kuwepo kwa viwango vidogo vya riba ya kukopa baina ya Tanzania na Nchi Wanachama;

**NA KWA KUWA**, kwa kuwa na sarafu moja, Umoja wa Fedha utaepusha athari za ubadilishaji wa fedha ndani ya Jumuiya na kuleta uwazi katika bei na hivyo kuongeza ushindani wa soko ndani ya Jumuiya;

**NA KWA KUWA** pamoja na Nchi Wanachama kukubaliana kurazinisha (harmonize) sera za bajeti, sera za fedha, na sera za ubadilishaji wa fedha za kigeni ili kurahisisha uanzishwaji wa Umoja wa

Fedha, Nchi Wanachama zitazingatia nidhamu ya kibajeti ili kutodhoofisha Umoja wa Fedha na kusababisha mdororo wa uchumi ndani ya Jumuiya;

**HIVYO BASI**, kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Itifaki hii kwa Tanzania na kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na pia umuhimu wa kuridhia Itifaki hii, Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Tano, kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, linaazimia kuridhia Itifaki ya Kuanzisha Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (Protocol on the Establishment of the East African Community Monetary Union) ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ili Tanzania iweze kuweka mazingira na mfumo bora na imara kifedha (monetary and financial stability).

Limepitishwa na Bunge leo tarehe 25 Juni, 2014

Dkt. Thomas D. Kashililah

**KATIBU WA BUNGE**